TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA

Taarifa kwa Umma

Tanzania International University (TIU)

Tume ya Vyuo Vikuu inapenda kuwataarifu wananchi na umma kwa ujumla kuwa, Tume imebaini kuwepo udahili katika chuo cha "**Tanzania International University (TIU)"** kilichopo Kimara Dar es Salaam. Tunapenda kuwajulisha kuwa chuo hiki hakina ithibati ya Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) inayokiruhusu kudahili wanafunzi katika kozi yeyote.

Chuo hiki kimekuwa kikijitangaza kuwa kinatoa kozi kwa ngazi za Vyeti, Stashahada na Shahada za fani mbalimbali na kwa taarifa tulizo nazo tayari waombaji wameshaanza kutuma maombi na hata kudahiliwa kwenye fani walizoomba. Tume ya Vyuo Vikuu haijatoa ithibati kwa chuo hicho inayokiruhusu kudahili wanafunzi.

Aidha Ithibati waliyopewa wamiliki ni ile ya awali ambayo

inawapa ruhusa ya kuanzisha utaratibu wa kuandaa mazingira ya uanzishwaji wa chuo tuu, na si kudahili wanafunzi. Kwa sasa Chuo hiki hakijakamilisha masharti hayo na hivyo hakina ithibati inayoruhusu udahili wa wanafunzi.

Hivyo basi, chuo hiki kwa sasa kinaendesha na kufanya shughuli zake kinyume cha sheria na taratibu zilizopewa na Tume ya Vyuo Vikuu. Kwa maantiki hiyo basi, Tume inatoa maagizo yafuatayo kwa wamiliki wa kinachojiita 'Tanzania International University':

1. Tume inawaamuru wamiliki wa chuo hiki kukifunga mara moja la sivyo hatua za kisheria zitachukuliwa.
2. Kuacha mara moja mchakato wowote wa uanzishwaji wa chuo mahali hapo mpaka watakapotimiza masharti ya uanzishwaji wa chuo kama yanavyojifafanua kwenye sheria ya vyuo vikuu ya mwaka 2005 na maelekezo ya Tume.
3. Wamiliki wa chuo hiki kuomba radhi Umma wa watanzania ikiwa ni pamoja na wadahiliwa kwa kuwadanganya pamoja na kuwarudishia ada na tozo walizokilipa chuo.
4. Kutoa matangazo kwenye vyombo vya habari yenye kukanusha uwepo wa ruhusa ya chuo hiki kudahili wanafunzi.

5. Kutoa mabango yote yanayoonyesha uwepo wa chuo hicho na yale yanayoelekeza kuwepo kwa chuo hicho mahala pale.
6. Tume haitambui udahili katika chuo hiki na hivyo haitotambua Vyeti, Stashahada, na Shahada zitakazotolewa na chuo hiki.

Mwisho, Tume inawataka wananchi kuwa makini na vyuo vya namna hii vinapojitokeza ili kuepika kupoteza muda na fedha zao. Endapo wana wasiwasi wa uhalali wa chuo chochote wasisite kupata uhakika toka kwenye Tume ya Vyuo Vikuu au mamlaka nyingine inayohusika.

Imetolewa na;

Katibu Mtendaji

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)

Aprili 12 2013